**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**686** **VITENDO VYA KUJIFUNZA KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 05 Mei 2014**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **40** na sehemu **B** na **C** zina alama **30** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Eleza mbinu nne za kumsaidia mtoto kutengeneza sentensi sahihi za Kiswahili.
2. Bainisha faida nne za kutumia michezo ya kuigiza katika kufundisha stadi ya kuzungumza.
3. Fafanua hatua nne za kumfundisha mtoto kusoma maneno yenye herufi zinazofanana.
4. Taja njia nne za kumsaidia mtoto kutambua sauti tofauti za vokali na konsonanti.
5. Eleza kwa kifupi faida nne za kutumia nyimbo na mashairi katika kujenga lugha.
6. Taja mbinu nne za kumfundisha mtoto kutafuta maana ya maneno mapya kutoka kwenye muktadha wa sentensi.
7. Fafanua faida nne za kutumia picha na vitu halisi katika ufundishaji wa Kiswahili.
8. Bainisha hatua nne za kumfundisha mtoto kueleza hadithi kwa kutumia picha.
9. Eleza njia nne za kumsaidia mtoto kuelewa dhana ya neno katika Kiswahili.
10. Taja mbinu nne za kumfundisha mtoto kuandika maneno mapya kwa kutumia sanduku la maneno.

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali mawili katika sehemu hii.

11. Fafanua changamoto tano zinazoweza kutokea wakati wa kumfundisha mtoto stadi za usomaji kwa kutumia hadithi.
12. Eleza faida tano za kumfundisha mtoto kusoma kwa pamoja.
13. Taja hatua tano za kumfundisha mtoto kuandika sentensi fupi kwa kutumia mbinu ya onesho.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili katika sehemu hii.

14. Eleza hatua tano za kumfundisha mtoto kutambua herufi "e" kwa kutumia zana halisi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

15. Bainisha faida tano za kutumia kadi za maneno katika ufundishaji wa Kiswahili.

16. Fafanua faida tano za kutumia mbinu ya vitendo katika kufundisha Kiswahili.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org